

Bodi ya Maji ya Taifa

Bodi ya Maji ya Taifa imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya Mwaka 2009. Bodi ya Maji ya Taifa ni chombo cha ushauri kwa Waziri wa Maji katika uratibu wa sekta mbalimbali kwa mipango ya pamoja ya uendelezaji wa Rasilimali za Maji na utatuzi wa migogoro ya Mabonde na maji shirikishi (maji ya kimataifa).

Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji atakuwa mjumbe na Katibu wa Bodi kwa nafasi yake. Bodi inakaa madarakani kwa kipindi cha miaka mitatu na kuweza kuteuliwa tena wamalizapo kipindi cha awali.

Wajumbe

Wajumbe wa Bodi wanatoka katika sekta zifuatazo, pamoja na

(a) Mwenyekiti

- (i) Kilimo (ii) Nishati (iii) Viwanda (iv) Mimitu (v) Mazingira (vi) Mifugo (vii) Ardhi (viii) Wanyamapori (ix) Madini (x) Umwagiliaji (xi) Uvuvi (xii) Miundombinu

(b) Mwakilishi wa serikali za mitaa (c) Mwakilishi wa sekta binafsi (d) Mwakilishi wa Asasi Zisizo za Kiserikali (AZAKI)

Majukumu ya Bodi ya Kitaifa

- (a) Kushughulikia suala lolote litakalowasilishwa kwao na Waziri au Sekta nyingine kuhusiana na uendeleo wa rasilimali za maji na kutoa mapendekezo yao kwa Waziri au Sekta husika.
- (b) Kushauri kuhusu vipaumbele vya uwekezaji na namna ya ugharimiaji wake, kuratibu na kuoanisha miradi inayofadhiliwa kutoka nje pamoja na miradi inayoweza kuwa na athari katika Rasilimali za Maji.
- (c) Ushauri katika kuoanisha mipango ya sekta mbalimbali kuhusu Rasilimali za Maji.
- (d) Ushauri kuhusu uratibu wa usimamizi na mipango ya bonde.
- (e) Ushauri kuhusu utatuzi wa migogoro kati ya Mabonde na Mabonde na ndani ya Mabonde.
- (f) Ushauri kuhusu vipaumbele vya uwekezaji.
- (g) Ushauri kuhusu uhamishaji wa maji toka bonde moja kwenda bonde jingine.

- (h) Ushauri kuhusu rasilimali za maji shirikishi.
- (i) Mapendekezo ya kurekebisha Sheria zinazosimamia rasilimali za maji.
- (j) Kushauriana na Mkurugenzi wa rasilimali za maji kuhusiana na mambo ya kiufundi.
- (k) Kutayarisha taarifa ya miaka miwili kuhusu hali ya Rasilimali za Maji.
- (l) Kufanyakazi nyingine za kiushauri kama watakavyoagizwa na Waziri.